# Kanisa MIS

## Mfumo wa Taasisi za Kidini

Taasisi yoyote inapaswa kuwa na mfumo wa kuaminika katika usimamizi wa taarifa na habari. Matumizi ya mifumo sahihi na yenye ufanisi katika taasisi yoyote inaweza kupunguza hadi asilimia sabini (70%) ya gharama za uendeshaji ukilinganisha na usimamizi ambao hauna mfumo unaoeleweka. Taasisi nyingi hazina mifumo fanisi ya usimamizi wa utendaji hivyo hutumia muda mrefu zaidi, huleta makosa kwenye taarifa na vilevile huongeza gharama za uendeshaji.

Vivyo hivyo usimamizi wa taasisi za kidini hauna tofauti na mara nyingi huonyesha ugumu zaidi kwaajili ya idadi kubwa ya makaratasina pamoja na uwepo wa idara zinazotegemeana kwa hali ya juu. Usimamizi wa taasisi hizi hutumia njia za peni na karatasi ambazo huongeza ugumu wa kazi na gharama.

Kanisa MIS, ni mfumo wa teknolojia wenye lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa taasisi za kidini ili kuongeza uwazi na uwezo wa kupata taarifa/ ripoti muhimu kwaajili ya washarika na uongozi kwa bei nafuu. Kanisa MIS inawapa wahusika uwezo wa kufanya maamuzi muhimu juu ya taasisi kutokana na uwezo wa kuzingatia shughuli muhimu zote katika taasisi za kidini na kutengeneza ripoti zake.

**Kanisa MIS, ni mfumo wa teknolojia wenye lengo la kuongeza ufanisi katika usimamizi wa taasisi za kidini ili kuongeza uwazi na uwezo wa kupata taarifa/ ripoti muhimu kwaajili ya washarika na uongozi kwa bei nafuu.**

Kanisa MIS imebuniwa baada ya utafiti wa kina ili kuelewa namna taasisi za kidini zinavyofanya kazi. Kutokana na ulewa huo, Kanisa MIS inawezesha kujumuisha idara zote muhimu zinazotegemeanza katika taasisi hizi.

**Kutokana na idadi kubwa ya makarasi na kutegemeana kwa idara tofauti katika taasisi za kidini, usimamizi unakuwa mgumu na wenye utata wa hali ya juu**

Kuziweka shughuli za muhimu katika taasisi za kiidini katika mfumo wa kidigitali unawawezesha viongozi kuweza kupata taarifa muhimu kwa harika zaidi na kupata uwezo wa ufanya maamuzi, mipango na kutabiri hali ya mbeleni ya taasisi.




Mchoro hapo juu unaonyesha hali ya kifedha ya taasisi na umejumuisha vipengele vya malipo ya ahadi, matumizi na mapato mengineyo.

**DataVision International LTD**
**(ICT, Statistics & Research, & Corporate Performance Management Consultants)**
Tel +255-22-2701845/6 ■ Fax +255-22-2701848 ■ info@datavision.co.tz ■ www.datavision.co.tz

# Kanisa MIS
## Mfumo wa Taasisi za Kidini




Kanisa MIS inakupa uwezo wa

### Kupata taarifa muhimu papo hapo

Uwezo wa kupata taarifa za taasisi kutoka kwenye idara tofauti ndani ya muda mfupi

### Kufuatilia kirahisi shughuli za taasisi

Mfumo wa Kanisa MIS unawapa viongozi kufuatilia utendaji wa shughuli na miradi ya taasisi kwa urahisi zaidi, kwa mfano: Ahadi Zilizoahidiwa na Ahadi Zilizotolewa

### Kupunguza gharama za uendeshaji

Kanisa MIS inazisaidia taasisi za dini kupunguza gharama za matumizi kutokana na kuchapisha idadi kubwa ya makaratasi pamoja na kazi za "peni na karatasi" ambazo hutumia muda mrefu.

### Kurahisisha usimamizi wa taasisi

Kutokana na uwezo wa kupunguza zaidi ya asilimia sabini (70%) ya idadi ya makaratasi katika taasisi, viongozi na wadau wanaweza kufanya usimamizi wa shughuli za taasisi ndani ya muda mfupi zaidi.

### Kupata taarifa na ripoti muhimu

Kanisa MIS ina uwezo wa kutoa taarifa muhimu kutokana na ngazi za uongozi ambazo husaidia kufanya maamuzi katika maeneo ya Fedha, Usharika, na mengineyo.

### Kurahisisha mawasiliano kati ya taasisi na washarika

Mfumo wa Kanisa MIS umeunganishwa na mfumo wa SMS Mtandao kwaajili ya mawasiliano ya haraka kati ya taasisi na washarika kupitia simu za mkononi.

**Baadhi ya wateja wa Kanisa MIS:**

- Wazo Hill Lutheran Church
- Msasani Lutheran Church
- Bethania Lutheran Church
- Ubungo Lutheran Church
- Ukonga Lutheran Church
- Kivule Lutheran Church
- Kimanga Lutheran Church
- Kipawa Lutheran Church

**DataVision International LTD**
**(ICT, Statistics & Research, & Corporate Performance Management Consultants)**
Tel +255-22-2701845/6 ■ Fax +255-22-2701848 ■ info@datavision.co.tz ■ www.datavision.co.tz